**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0786617866**

**Mkuu wa Shule 0786617866**

**Makamu Mkuu wa Shule 0622356248**

**Matron/Patron 0622352093**

**Shule ya Sekondari LUPIRO**

**S.L.P.288**

**Tarehe .10/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**………………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUPIRO HALMASHAURI YA ULANGA MKOA MOROGORO MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya **PCB/PCM**

Shule ya Sekondari **LUPIRO** ipo umbali wa Kilometa 1.5 Magharibi mwa Mji wa **IFAKARA** Usafiri wa basi kutoka mjini **IFAKARA** unapatikana katika kituo cha mabasi **KIBAONI** Nauli ni Shilingi **6000/=** kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 03/07/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023,

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 SARE ZA SHULE**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya bluu bahari na shati mbili za mikono mirefu zenye nembo ya shule (mbili), zinapatikana shuleni
ii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama, (unaweza kuipata shuleni)
iii. Sare ya Michezo ni track suti daki bluu (moja), jezi za daki bluu (moja) na pea ya raba rangi yeyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana;
vii. Sweta daki bluu (moja);
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni mbili kijivu unaweza kuipata shuleni)
ix. Tai mbili za blue bahari zinapatikana shuleni*;*
x. Tisheti (T-shirt) dark blue (moja) inapatikana karibu na shule kwa shs.15,000/=

### 2.2 Gharama mavazi yanayopatikana karibu na shuleni;-

a) Sketi shs. 27,000/= @ kila moja
b) Shati shs. 15,000/= @ kila moja
c) Tai shs. 5,000/=@kilamoja
d) Tracksuit shs. 22,000/= @ kila moja
e) Tisheti shs. 15,000/= @ kila moja
f) jezi shs. 12,000/=@kilamoja
g) Sketi shs. 27000/= @ kila moja
h) Shati shs. 15000/= @ kila moja
i) Shamba dress shs. 27,000/=@kila moja
j) Nusu kanzu + juba 35,000/= kwa kila moja
k) Sweta shs. 16,000/= kwa kila moja

### 2.3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari **11** counter book quire 3 au four

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kama, chands book kwa fizikia, biological science kwa biolojia,pure 1& 2, tlunter kwa hesabu.

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Godoro ft 2.5 kwa ft 6;

vii. Mashuka Jozi 2 pink, blanket 1 rangi yeyote, foronya ya godoro 1, chandarua 1 *rangi ya pink*

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

## 2.4 MICHANGO MBALIMBALI

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2.5 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

v. Faili la kutunza kumbukumbu za mwanafunzi

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule** **<u>ANNETH M. CHENGULA</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0786617866**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0622356248**
- **Mwandamizi Taaluma 0625135028**
- **Mwandamizi Malezi 0626614163**